

# HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA

SHULE YA SEKONDARI ITUMBA,  
S.L.P 153,  
**IGUNGA.**  
0629-188207

**Kumb.NA.ITSS/F.1.J.1.12.Vol.3/2020**

12/12/2020

MZAZI /MLEZI MWANAFUNZI:.....

SHULE YA MSINGI ATOKAKO:.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ITUMBA WILAYA YA  
IGUNGA MKOA WA TABORA MWAKA 2020**

## **1. UTANGULIZI**

Ninayo furaha kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Itumba ipo umbali wa KM 37 kusini kutoka makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya Igunga, Shule hii ni ya kutwa hivyo Mzazi /Mlezi anapaswa kumtafutia mwanae sehemu ya kuishi na chakula. Muhula wa kuanza masomo utaanza tarehe 11/01/2021.

## **2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

### **2.1 SARE ZA SHULE**

#### **Sare za shule kwa wavulana**

- (a) Suruali mbili rangi ya ugoro zenyne mifuko miwili pembedi na mmoja nyuma ziwe na marinda mawili tu kila upande
- (b) Shati mbili nyeupe za mikono mifupi (mpya)ziwe na urefu wa kutosha kuchomekea
- (c) Viatu vyeusi nya ngozi visivyo na visigino virefu pia visiwe na urembo wowote
- (d) Soksi nyeupe zisizo na urembo jozi mbili
- (e) Mkanda mweusi (wa ngozi)
- (f) Nguo za michezo
- (g) Sweta rangi ya ugoro

#### **Sare za shule kwa wasichana**

- (a) Sketi mbili rangi ya ugoro (kitambaa kizito)zenye mshono wa rinda box na urefu uzidi magoti kwenda chini inchi 3 (tatu)

- (b) Shati mbili nyeupe za mikono mifupi zenyenye urefu wa kutosha kuchomekea
- (c) Viatu vyeusi nya ngozi visivyo na visigino virefu bila urembo jozi mbili
- (d) Soksi nyeupe
- (e) Rangi ya Hijab ifanane na sare za shule
- (f) Nguo za michezo
- (g) Sweta rangi ya ugoro

## **2.2 VIFAA VYA DARASANI**

- (a) Daftari kubwa 9
- (b) Kalamu za wino (nyeusi na blue)na penseli moja
- (c) Mathematical set (Mkembe wa hesabu)
- (d) Rula moja sm 30
- (e) English –Swahili Dictionary
- (f) Mkoba (begi)kwa ajili ya kubebeara daftari

## **3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995.Aidha nazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elim,Sayansi na Teknolojia,yenye dhamana ya elimu nchini na unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo utafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada a kuripoti shulenii.

- (a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shulenii lazima
- (c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation)
- (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuweka ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na maizngira ya shule
- (g) Kuvalaa sare ya shulke wakati owte unapotakiwa
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- (i) Kutunza mali za umma

**NB:**Ukibainika kufanya uhalifu wa mali ya shule/Umma mzazi/Mlezi awajibike kulipa mali hiyo.

## **4. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

- (a) Wizi
- (b) Uasherati na Ushoga
- (c) Ubakaji

- (d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyia kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi,kubeli na kadhalika
- (e) Kupigana au kupiga
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- (g) Kudharau Bendera ya Taifa
- (h) Kuwa mjamzito /kupata mimba
- (i) Kuoa au kuolewa
- (j) Kutoa mimba
- (k) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki uvuruga amani na usalama wa shule au watu
- (l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- (m) Kuwa na simu ya mkononi

**5. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAPASWA KUKAMILISHWA NA  
KUWASILISHWA SHULENI NA WANAFUNZI**

- (a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali  
Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shulenii
- (b) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria ,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

Mimi Mzazi wa .....Nakiri  
kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Jina la Mzazi.....

Saini ya mzazi .....

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

.....

**CHONJA B CHARLES**

**MKUU WA SHULE**

# **HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA**

## **SHULE YA SEKONDARI ITUMBA**

(Uende na fomu hii kwa Mganga wa Hospitali ya Serikali kwa ajili ya vipimo)

**MGANGA/DAKTARI**

**HOSPITALI YA.....**

**Tarehe .....**

**S.L.P .....**

## **MEDICAL CERTIFICATE**

Jina la Mwanafunzi.....kidato.....umri.....

### **Afyah yake kwa ujumla**

- (a) Kifua .....
- (b) Masikio .....
- (c) Macho .....
- (d) Akili .....
- (e) Kilema chochote kitaje.....
- (f) Mkojo.....
- (g) Choo(stool).....

1. Kwa wasichana tu.Nimemwona anamimba/hana  
mimba.....  
Mengineyo .....
2. Nimempima mtajwa hapo juu na nimewona amepatikana na  
ugonjwa.....
3. Nimempima mtajwa hapo juu na nimemona anaweza/hawezu kusoma kwa  
sababu.....  
.....

.....

.....

**JINA NA SAHIHI YA MGANGA**

**CHEO**